**3 JUNI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Arobaini na Mbili — Tarehe 3 Juni, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Arobaini na Mbili.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali; tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Sasa ninamwita Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Katavi, aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba.

Na. 496

**Ujenzi wa Miundombinu Shule ya Sekondari Mkondo wa Amali – Katavi**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. THOMAS K. MAGANGA** aliuliza: -

Je, lini miundombinu ya Shule ya Mkondo wa Amali Mulele itajengwa ikiwemo nyumba ya walimu na karakana za ufundi wa magari na umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo J. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka 2023/2024 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya amali katika Halmashauri ya Mlele ambapo shule hiyo imejengwa katika Kata ya Utende. Miundombinu iliyojengwa ni pamoja na madarasa nane, jengo la utawala moja, maktaba moja, maabara mbili, chumba cha TEHAMA kimoja, bwalo moja, mabweni manne, karakana moja, nyumba ya mwalimu moja, matundu ya vyoo nane, kichomea taka kimoja na tanki la ardhini kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa shule hii umekamilika na shule imesajiliwa kwa jina la Shule ya Sekondari Mgombe Amali ya Kihandisi. Shule hii ina wanafunzi 63; wavulana 38 na wasichana 25 wanasoma amali za ufundi bomba, ufundi magari, ufundi umeme na magari na mfumo wa umeme wa jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga shule za amali ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma masomo ya amali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, maswali ya nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo shule ya amali ambayo inajengwa katika Jimbo la Mlalo pale Tarafa ya Mlalo katika Kata ya Mwangoi. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa shule ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mpango wa kupeleka shule za amali katika majimbo ambayo hayakufanikiwa kupelekewa Vyuo vya *VETA*. Je, uko mpango wa kupeleka shule mahsusi ya ufundi kwa maana ya amali katika Jimbo la Bumbuli? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali kupitia Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 imeweka mkakati madhubuti kuhakikisha kwamba tunaboresha elimu ya sekondari kwa maana ya mafunzo ya amali na kihandisi na ndio maana Serikali imeanzisha shule 103 na kati ya shule hizo, shule 29 ni za amali za kihandisi, lakini shule 74 ni za mafunzo ya amali kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameongelea shule ya amali katika Jimbo la Mlalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilipeleka fedha awamu ya kwanza takribani shilingi milioni 583 kwa ajili ya ujenzi wa majengo awamu ya kwanza na majengo hayo kote nchini yamekamilika na yako machache yako hatua za mwisho za ukamilishaji, na hatua inayofuata ni ujenzi wa awamu ya pili. Serikali inaanda taratibu za kibajeti kwa ajili ya kupeleka fedha ili tuweze kukamilisha majengo hayo.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Sekiboko kwamba tutahakikisha pia jengo au shule ya amali katika Jimbo la Mlalo

linapelekewa fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuhusiana na ujenzi wa shule za amali kwenye majimbo ambayo hayana *VETA* ikiwemo Jimbo la Bumbuli, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea. Kwanza kufanya tathmini, lakini pili kuendelea kuainisha maeneo ambayo ni muhimu kujengewa shule za amali na tutahakikisha pia tunatoa kipaumbele katika Jimbo la Bumbuli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alan Mvano, swali la nyongeza.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na mimi nipongeze jitihada hizi nzuri za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 Wilaya ya Kakonko 60% ilionesha kuwa na watoto, 30% vijana na 10% wazee. Sasa kwa muktadha huo katika Wilaya ya Kakonko hatuna shule ya amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi sasa mpango wa Serikali kwa kuzingatia kundi hili kubwa la 60% ya wananchi wa Kakonko ambao bado ni watoto wa kujenga shule ya amali katika Wilaya ya Kakonko ili kuweza kuwajengea uwezo na kuhakikisha wanakuwa wakiwa na elimu bora katika mazingira yetu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa shule za sekondari za amali kwanza Serikali ilitoa kipaumbele kwa halmashauri au wilaya ambazo hazina Vyuo vya *VETA*, lakini kwa sababu ya dhamira njema ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sasa wilaya zote zinaendelea na ujenzi wa *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa muktadha huo tuna uhakika kwamba Wilaya ya Kakonko pia itapata Chuo cha *VETA* lakini wakati huo huo tutaangalia uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga shule za amali katika Jimbo la Kakonko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Shule ya Sekondari ya Ihanda ilichaguliwa kuwa ni mojawapo ya shule ambayo ingeweza kujengewa miundombinu ya mafunzo ya amali. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kuanza kujenga miundombinu hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ziko shule ambazo zimekwishaainishwa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Vwawa kwamba tuna mpango wa kuendelea kuandaa bajeti kwa awamu ili kuendelea kujenga majengo yatakayoziwezesha baadhi ya shule kupata hadhi ya kuwa pia na mafunzo ya amali.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuipa kipaumbele shule hiyo kwa kadri ya bajeti zetu na kwa kadri ya tathmini ya vigezo ili tuweze kuona uwezekano wa kuongeza majengo ya mafunzo ya amali katika shule hiyo ya sekondari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Kahama Mjini, aweze kuuliza swali lake.

**3 JUNI, 2026**

Na. 497

**Ujenzi wa Barabara za Ndani Kahama**

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA** aliuliza: -

Je, lini barabara za ndani katika Jimbo la Kahama Mjini zitajengwa kwa kiwango cha lami na changarawe ili kuepuka adha ya usafiri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Jimbo la Kahama Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ujenzi wa barabara katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imetenga kiasi cha shilingi milioni 600 na mwaka 2026/2027 kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ina mpango wa kujenga kwa kiwango cha changarawe barabara zenye urefu wa kilometa 51.43 kwa gharama ya shilingi milioni 716.95. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imepanga kujenga barabara za ndani zenye urefu wa kilometa 58.5 kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 767.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya uboreshaji wa barabara za ndani na Manispaa ya Kahama kwa kiwango cha lami na kiwango cha changarawe ili ziweze kupitika wakati wote. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benjamin Ngayiwa, swali la nyongeza.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali lakini nipende tu kuweka swali la nyongeza kwamba Mji wetu wa Kahama umekuwa ni mji ambao unakuwa na changamoto kubwa sana ya kupitika kwa barabara hasa wakati wa masika, Kata ya Majengo, Kata ya Mhungula, Malunga, Nyahanga, Nyasubi, Mhungula na hasa ile barabara ya kuelekea kwenye machimbo kule Mwine ambayo inaingiza fedha nyingi sana Serikalini bado zinakuwa hazipitiki wakati wa mvua.

Sasa nini mpango wa Serikali kwenda kuongeza bajeti ya ujenzi wa barabara za lami kutoka kilometa moja kwa kila mwaka twende kilometa tatu kwa kila mwaka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Jimbo la Kahama Mjini kwa namna ambavyo amekuwa mwakilishi madhubuti sana wa wananchi wa Jimbo la Kahama Mjini, na mimi nimhakikishie kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutahakikisha tunampa ushirikiano wa kutosha ili barabara za Jimbo la Kahama Mjini ziweze kupitika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika majimbo na manispaa ambazo zimetengewa fedha nyingi kwa ajili ya uboreshaji wa barabara za changarawe na lami Jimbo la Kahama Mjini ni moja ya majimbo hayo. Kwa mfano, kupitia Mradi wa *TACTIC* hivi sasa ambao tayari tumeshasaini mkataba na kazi zinaanza kuendelea tayari tumetenga shilingi bilioni 22.31 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami Kahama Mjini, kilometa 16.58 ambazo zitajengwa katika maeneo ya eneo la mjini kilometa 12.13, eneo la viwanda

Zongomera kilometa 3.08, eneo la kituo cha mabasi na soko kilometa 1.37. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 tumetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami kilometa moja, lakini pia tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za changarawe zaidi ya kilometa 58.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imedhamiria kuhakikisha kwamba Manispaa ya Kahama inakuwa na barabara bora za lami na changarawe na tutaendelea kutenga fedha ili ziweze kujengwa na kuwa na huduma nzuri ya usafiri katika Jimbo la Kahama Mjini.

**MWENYETI:** Mheshimiwa Mbwilo Kapunda, swali nyongeza.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na neema ya mvua ambayo Wilaya yangu ya Nkasi imepata katika msimu huu imepelekea barabara zote za pale Mjini Namanyere kuharibika sana. Sasa mvua imeisha; je, ni lini Serikali itatuwezesha kujenga hizo barabara zilizoharibika vibaya? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara alishakuja Ofisi za Waziri Mkuu, TAMISEMI mara kadhaa na tumemhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kufuatia mvua hizi nyingi barabara zetu zimaharibika za Jimbo la Nkasi Kaskazini, Wilaya ya Nkasi kwa ujumla lakini pia katika eneo la Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie kwamba tayari Serikali tumeshatoa maelekezo kwa Mameneja wote wa *TARURA* kote nchini, *TARURA* Mkoa na *TARURA* Wilaya wanaendelea na utangazaji wa zabuni wa 60% ya bajeti kwa ajili ya matengenezo ya haraka na ya dharura kwa barabara zote zilizoathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumsisitiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Nkasi kuongeza *speed* na kufika pia Namanyere na kuona barabara zilizoharibika ili ziweze kupata kipaumbele kwenye bajeti ambayo tayari tumetangaza kwa ajili ya kupata wakandarasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nipate kuuliza swali la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Songea Mjini kupitia Liwena, Kijiji cha Lipaya hadi kufika Mpitimbi ambapo inaunganika na barabara ile ya Likuyufusi - Mkenda ni barabara ya miaka mingi sana, na barabara hii haijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu na sasa tunavyozungumza daraja linalounganisha vijiji hivi limekwishaanza kukatika.

Je, ni lini sasa Serikali itaijenga barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Komba, Mbunge wa Jimbo la Peramiho kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara na nitumie nafasi hii kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Peramiho

kwamba kipaumbele cha Serikali kwenye miradi ya barabara ni kuhakikisha maeneo yote korofi yanajengwa ili wananchi waweze kusafiri na kusafirisha bidhaa zao bila kikwazo vyovyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nitumie nafasi hii nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Songea wafike kwenye barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja kutoka Songea kwenda maeneo mengine ili waifanyie tathmini. Kwanza, wajiridhishe na hali ya daraja hilo kama linaweza likafanyiwa matengenezo kabla halijaharibika, tuweze kufanya matengenezo ya dharura ili daraja hilo lisikatike, lakini tuone gharama zinazohitajika kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo ambayo haijatengenezwa muda mrefu ili Serikali iweze kutenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitakaowataja kuwapa nafasi ya maswali ya nyongeza, ninaomba maswali yawe kwa kifupi na maswali yaendane na swali la msingi.

Wabunge wafuatao wajiandae Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mheshimiwa Zuberi Mfaume, Mheshimiwa Ibrahim Shayo, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava na Mheshimiwa John John Nchimbi. Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Barabara inayotoka Kata ya Nyankende inapita Nyambeshi, Kata ya Bulungwa, Sabasabini, Kata ya Mpunze inayotuunganisha na Manispaa ya Kahama haipitiki kabisa na ndio inayolinda uchumi wa Halmashauri ya Ushetu.

Ni nini mkakati wa Serikali kuifanyia marekebisho ya dharura hiyo barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko barabara nyingi ambazo

zimeathirika na mvua nyingi zilizonyesha msimu ulipita na tayari mkakati wa Serikali umeanza kutekelezwa ambao ni kutangaza zabuni, kupata wakandarasi kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara zote zilizokatika na kuharibika zile barabara muhimu sana ambazo ni uti wa mgongo wa maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo barabara hiyo inaunganisha Ushetu na Kahama ni barabara muhimu na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari Meneja wa *TARURA* wa Shinyanga lakini pia wa Wilaya ya Kahama na Ushetu wameshatangaza zabuni, tutapata wakandarasi hivi karibuni kwa ajili ya kufanya marekebisho kwenye barabara hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi ninatokea Jimbo la Morogoro Kusini, ningependa kujua Barabara ya Kilengezi, Kongwa hadi Lukooni lini itaanza kutengenezwa ipo kwenye hali mbaya sana? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ziko barabara na hususani katika Jimbo la Morogoro Kusini ambalo lina neema ya mvua nyingi sana na kila msimu wa mvua barabara nyingi zinaathirika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mheshimiwa Zuberi, kwamba Serikali inaendelea kwanza tumeshafanya tathmini ya barabara zote zilizoharibiwa na mvua na tumeshapata gharama ya fedha ambazo zinahitajika takribani shilingi bilioni 300 na hivi sasa Serikali inaendelea na taratibu za kibajeti kwa ajili kuanza kupeleka fedha kwa utaratibu wa dharura, lakini pia utaratibu wa kibajeti ili kurekebisha barabara hizo.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa awamu tutahakikisha tunaendelea kufanya matengenezo katika barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ibrahim Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, kuna Mradi wa *TACTIC* wenye gharama ya shilingi bilioni 22.9 barabara ya kilometa 13.3 ambao uko Mjini Moshi. Mradi huu mkandarasi anautengeneza kwa kusuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli Serikali kuhusu mradi huu kuweza kwenda kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *TACTIC* katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa Mheshimiwa Mbunge Ibrahim ni moja ya miradi 45 inayotekelezwa na Serikali, na ni kweli kwamba tumekwishapata mkandarasi lakini utekelezaji au kasi ya utekelezaji wa mradi ule hairidhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kupitia *TARURA* tumekwisha mwelekeza; kwanza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, lakini na timu yetu ya wataalam ikae na mkandarasi mapema iwezekanavyo tuweze kuona nini changamoto ya mkandarasi ili tuweze kuchukua hatua ikiwemo na ikiwezekana kuvunja mkataba kwa kadri ya vifungu vya mkataba au kuhakikisha anaanza kufanya matengenezo ya barabara hiyo ili iweze kukamilika kwa mapema iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Solwa, Kata ya Salawi kuna *center* inaitwa Pango ni *center* ambayo ipo *busy* sana kwa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili uwe na taa za barabarani kufanya biashara usiku ni lazima kuwe na lami; je, ni lini mtatuwekea walau kilometa tano za lami katika Mji wa Salawi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imeendelea kufanya tathmini ya miji yetu midogo inayoibuka na kuweka mipango ya kuiboresha miji ikiwemo utaratibu wa kupendezesha miji yetu na moja mpango huo ni kuhakikisha kwamba tunajenga angalau vipande vya barabara za lami, lakini kuweka taa za barabarani ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi ikiwezekana hata usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Mnzava tumepokea hoja ya mji huo na tutamtuma Meneja wa *TARURA*, Mkoa wa Shinyanga na Meneja wa Wilaya wafanye tathmini, watuletee makadirio ya angalau kilometa chache za lami na ili tuweze kuona uwezekano wa kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kujenga barabara na kuweka taa za barabarani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Nchimbi swali la nyongeza.

**MHE. JOHN J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nilikuwa ninaomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu tuliokuwa nao wakandarasi wa kigeni wanapofanya kazi za ukandarasi hapa nchini mara zote kwenye mikataba yao huwa wanawekewa sehemu ya *interest* pale ambapo wanachelewa kulipwa, lakini wakandarasi wa Kitanzania kwenye mikataba yao ya *TARURA*

kipengele hicho hakipo na hivyo kupelekea wengi sana wanafilisiwa na mabenki pale malipo yanapochelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali wa kulinda wazawa ili waweze kukua na wenyewe wakawa na nguvu kama wakandarasi wa nje wanaolindwa na Serikali yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Jimbo la Nyasa, Mheshimiwa John John Nchimbi amekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa masilahi ya wakandarasi wa ndani ya nchi na mimi nimhakikishie kwamba hicho ni moja kipaumbele cha Serikali, kwanza kuhakikisha kwamba wakandarasi wa ndani ya nchi wanapata miradi na kiwango cha miradi wanayopata kilipandishwa mpaka shilingi bilioni 50, wakandarasi wazawa wanaweza kupata miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu zipo changamoto za kisheria za hapa na pale ambazo ni utaratibu wa kuendelea kuziboresha kwa kadri ambavyo tunazi-*experience* katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nichukue *observation* Mheshimiwa Mbunge ya kuhusiana na kifungu cha *penalty* kwa wale wakandarasi wa nje na wa ndani na Serikali itaendelea kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kufanya maboresho ili kuweka mazingira na uwanja mzuri kwa wakandarasi wa ndani kupata tija na faida katika miradi ya maendeleo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daudi Njalu, swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi; nilitaka kuuliza kwa Mheshimiwa Waziri

barabara zetu nyingi zimeathiriwa sana na kipindi hiki cha mvua hasa kwa maeneo yetu ambayo tunazalisha mazao ya kwenda kupeleka sokoni maeneo ya Mahembe, Kinamweli, maeneo ya Laini Chinameli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inayo mkakati gani wa kutoa fedha kukamilisha maeneo hayo ili wananchi waweze kuuza mazao yao kwenye masoko yaliyo mazuri wapate bei nzuri zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Itilima, Mheshimiwa Njalu Silanga kwamba barabara zetu nyingi za vijijini ni barabara muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi kwa ajili ya usafirishaji wa mazao lakini pia na usafiri kwa shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali kupitia *TARURA* tumeendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo, lakini jambo kubwa tumeendelea kuweka mipango ya kuzipandisha kutoka barabara za udongo kwenda barabara za changarawe na hatimaye kwa awamu kuwa barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Njalu kwamba tunafahamu barabara za Jimbo la Itilima zipo zilizoathirika na mvua na Serikali ipo kwenye taratibu kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo na tunaendelea kutangaza zabuni zetu 60% ya bajeti mameneja wa mikoa na wilaya wanaendelea. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba barabara hizo zitafanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo kubwa pia Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji wa aina (*design)* mpya ya barabara ambazo zitaweza kudumu kwa muda mrefu ili

kuepusha Serikali kurudia kujenga barabara hizo kila mwaka na kuitia hasara Serikali, lakini na jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo tunaendelea kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Destery Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa barabara ya Kabila – Ndobora – Kabale - Mahaha ina miaka mitatu bila kutengenezwa na imeharibika sana; ni lini Serikali itatoa fedha za dharura ili iweze kutekelezwa hiyo barabara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Kiswaga amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na hizo barabara za Jimbo la Magu, lakini kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu na haijafanyiwa matengenezo kwa zaidi ya miaka mitatu, bila shaka barabara hiyo ni kipaumbele cha hali ya juu katika Jimbo la Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitumie nafasi hii nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Mwanza na Wilaya ya Magu waipe kipaumbele barabara hiyo kwenye hii 60% ya zabuni ambazo zinatangazwa ili iweze kufanyiwa matengenezo na kurudi kwenye hali yake ya ubora zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Festo Dugange, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Baraka Ulimboka Mwamengo, kwa niaba Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

Na. 498

**Hitaji la Gari la Kubebea Wagonjwa**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya Ipinda?

**MWENYEKITI**: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Seif.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Baraka Ulimboka Mwamengo, Mbunge wa Jimbo la Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji mkubwa wa magari ya kubebea wagonjwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 hadi sasa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI imepokea jumla ya magari ya kubeba wagonjwa 382 na magari 212 ya uratibu na usimamizi wa shughuli za afya. Magari hayo yamepelekwa kwenye mikoa na halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilipokea gari moja la uratibu na usimamizi wa shughuli za afya na magari mawili ya kubebea wagonjwa ambapo gari moja lipo Kituo cha Afya Kilasilo na lingine Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Kwa sasa Kituo cha afya Ipinda kinahudumiwa na gari la wagonjwa lililopo Hospitali ya Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili kuendelea kununua magari ya kubebea wagonjwa na kuyapeleka kwenye halmashauri zenye upungufu ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikienda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali na sisi tunaona juhudi ya Serikali namna ambavyo inajali wananchi hasa pale wanapokuwa wanaumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali; Wilaya ya Kyela ina upungufu wa madaktari, lakini pia hata ma-*nurse*. Ni lini Serikali italeta madaktari wa kutosheleza Wilaya ya Kyela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na swali hilo, mimi kama Mbunge wa Mkoa wa Mbeya wa Viti Maalum hilo tatizo lipo hata Wilaya ya Mbarali, Chunya, Rungwe, *Mbeya DC* lakini pia lipo pamoja na Kyela yenyewe. *(Makofi)*

Sasa je, ni lini Serikali itatoa tatizo hilo lote kwa ujumla wake ili wananchi wanapokuwa wanaumwa wapate huduma kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na ameongea kwa niaba ya mkoa kwa sababu ni Mbunge wa mkoa anafahamu changamoto za mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuajiri madaktari na mwaka wa fedha uliopita ambapo Mheshimiwa Rais aliridhia vibali 5,000 vya madaktari na wataalam wetu wa afya (wauguzi) na tukawasambaza kwenye halmashauri zote nchini na kwa wastani kila halmashauri ilipata angalau wataalam 100 mpaka 200 ili waende wakatoe huduma ambazo Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaahidi wapiga kura wetu, wananchi wa Tanzania kwenye kampeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tutaendelea kutekeleza ahadi ambazo Mheshimiwa Rais ambazo amezitoa kwenye kampeni kuhakikisha tunapeleka madaktari wataalam ili waende wakatoe huduma zetu na kupunguza *referral* ambazo sio za lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mkoa kwamba tutaendelea kutenga wataalamu wetu na kuwapeleka katika maeneo hayo ili waende wakatoe huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Tarafa ya Mwese na Kituo cha Afya cha Mwese, Katuma hakina gari ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itapeleka gari kwenye tarafa hiyo ili kuokoa wananchi ambao wanapata shida na adha kwenye vituo hivyo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kupeleka magari kwenye halmashauri zetu hasa zile ambazo zina upungufu mkubwa wa magari na awamu hii inayofuatia tutaendelea kupeleka magari hasa kwenye zile halmashauri ambazo hazikupata kwa awamu iliyopita ili kuona namna gani zinaendelea kutoa huduma kwa mama zetu hasa wale wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kutoa taarifa na tunaendelea kuwapa wakurugenzi wetu lakini pia ma-*DMO* kuendelea kutumia ile huduma ya *M-Mama* ambayo Serikali inashirikiana na Vodacom kuhakikisha kwamba unaweza ukapata gari binafsi na likaenda likabeba ugonjwa wetu hasa kutoka ngazi ya afya ya msingi au katika kaya na kuwapeleka katika vituo vyetu vya afya na halmashauri zimekuwa zikilipa magari hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba tutaendelea kuangalia upungufu hasa katika maeneo ya halmashauri ambazo zina upungufu wa magari na kuziongezea magari hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sara Msafiri, swali la nyongeza.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza ninaishukuru sana Serikali kwa kutupa gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Mziha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za kijiografia kwenye Jimbo la Mvomero bado tunahitaji Serikali itusaidie kuleta gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Mlali, Mgeta na Kibati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, lini Serikali italeta magari hayo ili kusaidia huduma hii ya afya iweze kufanya vizuri kwa wananchi wa Mvomero?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Mvomero na tulifanya ziara ile siku ya Muungano katika jimbo lake na wananchi wanampenda kweli kweli kwa

sababu ikitokeza kwa wingi ili kushuhudia ile ziara na kutupa moyo watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kutenga bajeti ya kuongeza magari kadri ambavyo tunayapata kutoka Wizara ya Afya ili kuona namna gani tunaendelea kuwasaidia mama zetu, wagonjwa katika Jimbo la Mvomero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie ushirikiano kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kadiri ambavyo tunapokea magari na sisi tutaelekeza hasa kwenye halmashauri ambazo zina upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adonis Alfred, swali la nyongeza.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba Wilaya ya Muleba Serikali imejenga hospitali ya wilaya, lakini pia katika Jimbo la Muleba Kaskazini Serikali imejenga Kituo cha Afya cha Izigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivyo vya kutoa huduma za afya havina magari ya kubeba wagonjwa. Je, ni lini Serikali itapeleka nagari ya kubebea wagonjwa katika vituo hivyo vya kutoa huduma ya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Muleba Kaskazini kama alivyoliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaifahamu jiografia ya Mkoa wa Kagera na mimi nimepata kusoma kule, kwa hiyo, nafahamu mazingira yalivyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kutenga bajeti kuangalia magari haya kadri tunavyoyapokea ili tuyaelekeze katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ni kuendelea kuboresha miundombinu na kupeleka wataalam madaktari katika hospitali zetu hizo na hasa ule ujenzi wa hizi *maternity complex* za kisasa ili zile huduma ambazo zinahitaji *referral* ziweze kutibiwa katika vituo vyetu na waweze kupata huduma hizo ili wasihitaji zaidi haya magari ya *ambulance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye maeneo yale ambayo hawana huduma kabisa tutaelekeza magari yetu haya ya *ambulance* kadri tunavyo yapokea ili yaende kutoa huduma kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Azza Hamad, swali la nyongeza.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kituo cha Afya cha Tinde kilichopo Jimbo la Itwangi kiko barabara kuu na kinahudumia kata 10 ndani ya tarafa moja na watu mbalimbali wanaotoka maeneo tofauti kwa sababu ya maeneo kilichopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Tinde lilipata ajali mbaya sana zaidi ya miaka mitano sasa na halijaweza kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itatuletea gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Tinde?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Azza, Mbunge wa Jimbo la Itwangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Jimbo la Itwangi lina kata 14 na lina upungufu wa vituo vya afya, kwa hiyo, tukipelekea Mheshimiwa Mbunge gari la *ambulance* angalau wataweza kusaidia zile kata ambazo hazina vituo vya afya ili kuwahisha wagonjwa wetu katika Kituo cha Afya cha Tinde na kituo hiki kiko barabarani kwa hiyo kuna muda ambao tunapata zile ajali na wanahitaji msaada wa *ambulance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali tunafahamu changamoto hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI tunaenda kukupa ushirikiano Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba tunapeleka gari la wagonjwa hili liende kusaidia wagonjwa wetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Jimbo la Lulindi kwenye Kata ya Mkululu na Kata ya Namwanga kuna vituo vya afya ambavyo vinahudumia maeneo makubwa sana katika jimbo hilo, lakini havina magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini mtapeleka magari ya wagonjwa katika vituo hivyo viwili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilijibu kwenye swali la msingi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Mchungahela

kwamba tutaendelea kupeleka magari kwenye halmashauri hasa zile ambazo zina upungufu mkubwa na zipo pembezoni zaidi na zina uhaba mkubwa wa wataalam wetu ili kuhakikisha kwamba wagonjwa wetu wanaohitaji huduma hizi wawahishwe katika vituo ambavyo vinatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mchungahela nikuhakikishie katika maeneo ambayo umeainisha na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI tutaendelea kupeleka magari haya ili yaende yakaokoe maisha ya wagonjwa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Jafar Seif, Naibu Waziri - TAMISEMI tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha; sasa ninamwita Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 499

**Kulinda Biashara na Mitaji ya Vijana Dhidi ya Ucheleweshaji wa Malipo**

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO** aliuliza: -

Je, hatua gani zimechukuliwa kulinda biashara na mitaji ya vijana dhidi ya ucheleweshaji wa malipo ya madeni ya wakandarasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa niaba ya Wazir wa FEdha ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, Mbunge wa Viti maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitekeleza hatua mbalimbali za kuongeza na kulinda ushiriki wa vijana katika biashara. Kupitia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika MUDA WA KATI (2026/2027 – 2027/2028), Maafisa Masuuli wa mafungu ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wameelekezwa kuzingatia mkakati wa kulinda wawekezaji wa ndani *(local content)* kwa kutoa kipaumbele cha kwanza katika zabuni, masharti ya mikataba na malipo ya hati za madai pamoja na kuweka msukumo katika *joint venture* kwa mikataba ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kuhakikisha kuwa wakandarasi na wazabuni wanalipwa, mwaka 2025/2026 Serikali imetenga bajeti ya shilingi bilioni 700. Kwa kipindi cha Julai hadi Februari, 2026 kiasi cha shingi bilioni 477.6 kimelipwa. Aidha, Serikali itaendelea kulipa madeni ya wakandarasi ili kulinda mitaji yao pamoja na kuwezesha kuendelea kushiriki katika ujenzi wa miradi ya maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timida Mpoki swali la nyongeza.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri katika nchi za Umoja wa Ulaya, taasisi zinazofanya kazi na Serikali zinapaswa kufanya malipo ya madeni ndani ya siku 30, lakini pia riba hulipwa moja kwa moja endapo malipo yatacheleweshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali yangu ipo tayari kuandaa *Prompt Payment Policy* ya Taifa ili kuhakikisha wazabuni, wakandarasi, wafanyabiashara hususan vijana na *SMEs*

wanalipwa ndani ya muda maalum unaotambulika kisheria ili kulinda mitaji ya vijana na wananchi wanaofanya biashara na Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri. majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nipongeze sana Mbunge wa Viti Maalum dada yangu Timida ambaye ni Mbaraza la Vijana wa Taifa kutokea Mkoa wa Mbeya kwa namna anavyoendelea kujenga hoja makini hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea kwenye swali la nyongeza, kwanza kabisa miongoni mwa vitu ambavyo hata Kamati yetu ya Bajeti imeweza kutushauri kama Wizara ya Fedha na kama Serikali imetushauri tuweze kupunguza angalau muda wa uhakiki wa madeni ya wazabuni na wakandarasi na watoa huduma mpaka kufikia siku 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi tumeweza kupokea, lakini siku hizi 21 zinaweza zikapungua au kuongezeka kutokana na sababu kadhaa ikiwemo ukamilifu wa nyaraka, aina ya madeni lakini pia ushirikiano wa wadau kwa maana wadai pamoja na wadaiwa, lakini pia umri wa deni pamoja na wigo wa deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali, kama ambavyo nimejibu kwenye swali langu la msingi, tumeendelea kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi pamoja na watoa huduma na mpaka kufikia Februari, 2026 zaidi ya shilingi bilioni 477.6 ambazo tayari wakandarasi hawa na watoa wa huduma wamekwishalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipaumbele vikubwa vya Serikali katika bajeti yetu ya mwaka 2026/2027, tumetenga na tumekubaliana kuwa na mkakati wa kutenga shilingi bilioni 100 kila mwezi kwa ajili ya kulipa madeni ya wakandarasi, watoa huduma pamoja na wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Morris Makoi, swali la nyongeza.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakandarasi wa nchi hii wanadai fedha nyingi kama ambavyo ametamka Mheshimiwa Waziri, lakini wakandarasi wa ndani hawaruhusiwi kudai malipo yao pamoja na riba, kinyume na wakandarasi wa nje ambao hudai malipo ya madeni yao pamoja na riba.

Je, Waziri ana kauli gani kuhusiana na madeni ya wakandarasi wazawa wanaodai madeni yao pamoja na riba ili na wao wanufaike au waepuke hasara kama ambavyo wenzao wa nje wanavyoepuka?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nikiri kama Serikali tumeendelea kulipa madeni yakiwemo madeni ya wakandarasi wa kigeni na madeni ya wakandarasi ambao ni wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwenye swali langu la msingi, kwanza hakuna upendeleo wowote baina ya wakandarasi wa nje na wakandarasi wa ndani, kama Serikali tumekuwa tukishamaliza kufanya uhakiki wa madeni hayo tumekuwa tukilipa kwa wakati na hivyo Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini nipende kukuhakikishia kwamba kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba madeni yote ya wazawa na wa kigeni yanalipwa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laurent Deogratius, Naibu wa Waziri wa Fedha tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa ni Wizara ya Kilimo, ninamwita Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, aweze kuuliza swali lake.

Na. 500

**Mradi wa Umwagiliaji – Arusha Chini**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji wa Arusha Chini utaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi David Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji nchini ikiwemo katika Mkoa wa Mtwara. Lengo la utekelezaji wa miradi hiyo ni kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuchangia kuongeza kipato cha wakulima kupitia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo, hadi kufikia Machi, 2026 mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji wa Arusha Chini amepatikana na kukabidhiwa eneo la mradi kwa ajili ya ujenzi. Mradi huo una ukubwa wa jumla ya hekta 264 ambapo gharama za utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo ni shilingi bilioni 14.83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wakulima 950 katika Vijiji vya Arusha, Arusha Juu, Mkomo, Ngorongoro, Chawi, Chawi Sokoni, Mchanje na Ngonja na hivyo kuwezesha wakulima kulima zaidi ya mara mbili kwa mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza na ushauri.

Kwa kuwa mkandarasi ameshapatikana na kwa kuwa mkandarasi ameshakabidhiwa eneo la mradi; je, ni lini mkandarasi huyo sasa ataanza kazi ya ujenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri, kwa kuwa mradi huu unajengwa pembezoni kabisa mwa Mto Ruvuma na kutokana na mabadiliko ya tabianchi, mkondo wa mto huu sasa unaanza kuhama na kuathiri vijiji vya jirani kama Maembe Chini. Ni ushauri wangu sasa wakati wa utekelezaji wa mradi huu, wataalam wa kilimo washirikiane na wataalam wa mazingira ili kuhakikisha yale maji ambayo yanaathiri wanakijiji yanatumika kwenye mradi na badala yake kwenda kuathiri makazi ya wanavijiji, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chikota, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Chikota kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa karibu masuala ya kilimo, sio kwenye jimbo lake tu, na nchi nzima. Kwa sababu tangu uhuru sote tunakubali kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu. Kilimo ndiyo kinatoa takribani 100% ya uhakika wa chakula kwenye nchi yetu, kinatuhakikishia usalama, malighafi kwenye viwanda, kinatoa ajira kwa vijana wa nchi yetu na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia ilani CCM maelekezo yake yeye mwenyewe sambamba na Dira yetu ya 2050 amethibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hali ya kilimo nchini ilivyokuwa mwaka 2020 na sasa ameamua kuongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294 mpaka shilingi trilioni 1.1 ili

kumnufaisha mkulima wa nchi hii, lakini pia Dkt. Samia kama haitoshi, kwa kutambua umuhimu wa eneo la umwagiliaji, miradi takribani 886 inatekelezwa nchi nzima, ikiwemo na miradi 146 ambayo mmojawapo ni wa kwake Mheshimiwa Chikota huu umeingizwa katika kundi hilo. Ipo miradi 28 ambayo inakaribia kukamilishwa, ipo miradi 71 ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali, na ipo miradi 48 ambayo wakandarasi wamekwishapatikana kinachosubiriwa sasa ni kupewa fedha waanze kujenga miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Chikota na wananchi wote wananyamba kwa ujumla wawe na Subira, maadam walimchagua Dkt. Samia Suluhu Hassan na maadam Mbunge wao ameshiriki kupitisha bajeti ya kilimo ya mwaka huu, tunawapa uhakika fedha zinatafutwa wanakwenda kulipwa, mjenzi anaanza kujenga mradi huo ili kuweza kuwafaidisha wananchi wa Arusha Chini na maeneo yote ambayo yametajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri, Serikali imepokea ushauri huo, tutaielekeza kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Tume yetu ya Umwagiliaji wakae na Mheshimiwa Mbunge wapokee ushauri wake, wauingize katika utekelezaji bila kuathiri sheria na kanuni za nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa ninamwita Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 501

**Kukamilisha Ujenzi wa Chuo cha *VETA* - Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilaya Biharamulo ili kuwezesha vijana kujikwamua kutokana na mafunzo yanayotolewa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Mheshimiwa Wanu Hafidh.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ninaomba kujibu swali namba 501 la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Biharamulo ni miongoni mwa vyuo 64 vya *VETA* vinavyojengwa na Serikali katika Mkoa na Wilaya ambazo hazina Vyuo vya Ufundi Stadi. Mradi huu unalenga kuongeza fursa za mafunzo na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Biharamulo unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026. Hadi sasa Serikali imetumia kiasi cha shilingi bilioni 1.12 kati ya shilingi bilioni 1.6 zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi huu na ujenzi wake umefikia 72%.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, maswali ya nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina hoja tu kama mbili ambazo ninazo na mradi huu ulianza mwaka 2023. Tumefanya *extension* tulitegemea umalizike mwaka 2024 lakini haujamalizika mpaka sasa. Kwa hiyo, tunajua nia njema ya Serikali, lakini miradi hii ya ujenzi kwanza inakuwa na mkandarasi anayejenga mradi unapochukua muda mrefu sana, unaongeza gharama kwa mkandarasi, lakini gharama hata kwa wananchi pale kwa sababu tulitegemea mradi huo uwe umemalizika na uanze kutoa huduma kwa wananchi. Kwa mfano kunakuwa na

zile *performance guarantee* na vitu vingine kama hivyo. Kila inapo-*expire* lazima mtu aende aka-*renew* tena maana huwezi kuendelea na mradi ukiwa nje ya *performance*. Sasa zote hizo ni gharama ambazo zinaongezeka, lakini tumekuwa na shida ya umeme pia pale, kwa sababu unahitajika shilingi milioni 90 ili umeme uweze kuingizwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa ninaomba kujua, *cash flow* si nzuri, ninataka nisikie kauli ya Serikali kuhusu *cash flow* ili tuweze kumalizia haya majengo ambayo yameshaanza, lakini shida kubwa ni umeme. Lile eneo halina umeme kabisa na eneo ambalo tumechukua sasa *stage* zinazofuata nyingi hazitaendelea bila kuwa na umeme.

Kwa hiyo, nilitaka kupata kauli ya Serikali, kama tunaweza kupata shilingi milioni 90 ile kwa haraka kwanza tuingize umeme ili hatua nyingine zinazoendelea za ujenzi wa kumalizia ziweze kufanyika hali kukiwa na umeme tayari pale. Maji tulishafikisha, lakini shida ni umeme. Ninaomba kusikia kauli ya Serikali juu ya hayo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba ujenzi huu wa vyuo hivi umechelewa, lakini kama tulivyosema katika bajeti ya Wizara ya Elimu kwamba fedha tayari zilishatengwa na tayari zimeanza kutoka, na fedha hizi zitaingia kwa awamu kwa kila chuo. Tayari nimeanza kupokea mrejesho kutoka baadhi ya vyuo kwamba tayari fedha hizi zimeanza kuingia na wanaendelea na ujenzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Ezra kwamba fedha itakuja, ujenzi utaendelea, na suala la umeme tutafuatilia pamoja mimi na yeye. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi (*Dodoma Polytechnic College)* katika Mtaa wa Lugala, Kata ya Mbalawala. Je, ni lini Serikali itaanza kuchukua wanafunzi katika chuo hicho ambacho kiko ndani ya Jiji la Dodoma?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chinyele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imekamilisha kwa kiasi fulani ujenzi wa *Dodoma Polytechnic,* na kama Mheshimiwa Mbunge anakumbuka vizuri tulifanya ziara pamoja katika chuo kile na hatua iliyofikia ni nzuri. Kwa hiyo, tu nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaenda kumalizia ukamilishaji wa chuo kile na matarajio ya mafunzo ni kuanza mwaka huu wa 2026/2027. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuishukuru sana Serikali, tumshukuru Dkt. Samia kwa kutupatia chuo kizuri na watoto wetu kuendelea kupata ujuzi na kujiongezea ajira kwenye maeneo yao, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, ulifika Chuo cha *VETA* Chemba. Tunakushukuru sana, tulikupa kilio chetu, ujenzi wa *fence* tunakushukuru umetupatia shilingi milioni 100, *fence* yetu imeanza. Ni lini sasa changamoto yetu ya pili ya uongezaji wa walimu

kwenye chuo kile ili watoto wetu waendelee kunufaika na uwepo wa chuo hicho ndani ya Wilaya yetu ya Chemba?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Majala, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Majala alifikisha changamoto hizi mbili na ile moja tayari imeanza kupata suluhisho, lakini nimuahidi kwamba kama vile ambavyo tume-*solve* hii changamoto ya kwanza, basi tunaenda kumalizia hii changamoto nyingine. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi, kati ya Vyuo vya *VETA* ambavyo vimepata bahati kimoja ni Chuo cha *VETA* Chemba. Kwa hiyo asiwe na wasiwasi, changamoto yake tunaenda kuimaliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wanu Hafidh, Naibu Waziri wa Elimu, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea ninaomba kuwatambulisha wageni walioko Bungeni ili kuruhusu wageni wengine waweze kuingia kwa kuwa ratiba yetu leo itaisha mapema.

Tunaanza na wageni wawili wa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ambao ni wafanyabiashara kutoka Kinondoni, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni saba wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ambao ni wanafunzi wanasoma Vyuo Vikuu Mkoani Dodoma wanaotokea Jimbo la Ludewa, Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 13 wa Mheshimiwa Johannes Lembulung' Lukumay ambao ni Konga kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 29 wa Mheshimiwa Mwanaenzi Hassan Suluhu ambao ni wafanyabiashara na wasusi kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni 53 wa Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Msingi Wilaya ya Karatu, Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 53 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, walimu na wanafunzi kutoka *Msimbazi Center,* Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 100 wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Awali na Msingi ya *Modern* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni pia waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 24 na walimu watano wa Shule ya Msingi ya *Bible Baptist* kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 42 na Mkuu wa Kitivo na Mkuu wa Idara ya Uchumi kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wetu wote karibuni hapa Bungeni, Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa ni Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninamwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero aweze kuuliza swali lake.

Na. 502

**Ujenzi wa Minara Halmashauri ya Mji Ifakara**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa minara ya mawasiliano Halmashauri ya Mji Ifakara hasa Ikwambi, Mang'ula B na Kanyenja?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeendelea kutekeleza miradi ya kuboresha Huduma za Mawasiliano katika Jimbo la Kilombero. Katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Tanzania ya Kidijitali, mnara wa mawasiliano wa mtoa huduma Honora *(Yas)* ulijengwa Kata ya Signal katika Kijiji cha Sagamaganga na unatoa huduma katika Vijiji vya Signal, Sululu na Sagamaganga. Aidha, kupitia awamu hiyo Kampuni ya Honora ilijenga mnara katika Kijiji cha Mhelule, Kata ya Mang'ula, unaohudumia vijiji vya Kanyenja, Mhelule, Mikoleko, Mang'ula A na Mang'ula B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo tarehe 8 Aprili, 2026, *UCSAF* ilifanya tathmini katika Vijiji vya Mang'ula B, Kanyenja na Kitongoji cha Ikwambi na kubaini kuwa Kijiji cha Kanyenja kilijumuishwa katika Mradi wa Mawasiliano ya Simu vijijini wa minara 636 ambapo mnara huo ulijengwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* katika Kijiji cha Kanyenja na unatoa huduma za teknolojia ya *2G* na *4G*. Aidha, Kijiji cha Mang'ula B na Kitongoji cha

Ikwambi vilibainika kuwa na changamoto za mawasiliano hivyo *UCSAF* itayajumuisha maeneo hayo kwenye miradi ya mawasiliano ya simu ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo katika Kijiji cha Mang'ula B na Kitongoji cha Ikwambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, maswali ya nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri na timu ya watu wa Wizara walifika jimboni kwangu, wakatembelea maeneo yote ambayo tuliomba minara. Tuliomba minara 10 na tumepewa minara nane, ni imani yangu kama majibu ya Serikali yalivyo, katika minara miwili ya Ikwambi na Mang'ula B basi itaanza kujengwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, katika minara hii nane ambayo tumeipata kuna tatizo la changamoto la usikivu mdogo, kwa mfano pale Lumemo, Ihanga kuna mnara lakini bado kuna changamoto ya mawasiliano. Je, ni lini mpango wa Serikali kupitia katika minara ambayo imejengwa ili sasa kuiongezea nguvu iweze kusikika vizuri kwa maana ya *2G* iende kwenye *4G*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini mpango wa Serikali wa mnara mmoja kutumika na kampuni zote utaanza, kama ambavyo Kamati ya Bunge tumeshauri? Sehemu ambako Tigo wamejenga tusianze kuhangaika kutafuta tena wengine wakajenge. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza

Mheshimiwa Asenga ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Wizara yetu. Amekuwa mtu hodari katika Kamati, mchangiaji mzuri na mshauri mzuri, hakika wananchi wa Kilombero wamepata Mbunge jembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nininaomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo; kuhusu minara iliyojengwa kwake kuwa na nguvu kidogo, hili tatizo huwa linatokea kutokana na inapojengwa baadaye watumiaji wanaongezeka na makazi yanaongezeka. Kwa hiyo, nguvu inapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kuifanyia tathmini minara hiyo, kugundua udhaifu uliopo na kuwasiliana na watoa huduma walioijenga hiyo minara ili waweze kuiongezea nguvu kulingana na tathmini itakayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, Serikali inaendelea na mkakati wake wa kujenga minara kupitia mkakati wa miaka mitano. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika maeneo yote ambayo tumeyagundua kwamba yana changamoto ya mawasiliano katika eneo lake tutayaingiza katika mpango wa Wizara wa ujenzi wa minara kwa mwaka ujao wa fedha wa 2026/2027. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Utaly.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipengele hicho cha kwamba mnara mmoja kutumika na mitandao yote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mnara mmoja kutumiwa na wafanya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, tafadhali.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Swali langu la pili ndilo lilikuwa hilo, la kwanza amejibu vizuri, la pili nilisemea kuhusu mnara mmoja kutumika na mitandao yote.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mnara mmoja kutumiwa na watoa huduma wengi au *roaming,* tunaendelea na mazungumzo, *TCRA* inafanya mazungumzo na watoa huduma ili kuwezesha huduma hii kwamba mnara mmoja unatumiwa na watoa huduma wengi. Baadhi ya mashirika kama...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa, wewe zima hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTCL* na *Airtel* wameshaanza hiyo huduma. Tunaendelea kufanya mazungumzo na watoa huduma wengine ili hili liwezekane kwamba mnara mmoja kutumiwa na watoa huduma wengi.

Kwa hiyo, nitumie nafasi hii pia kupitia Bunge lako Tukufu kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kuharakisha hayo mazungumzo ili mpango huu uanze kutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Utaly, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, niwashukuru sana wizara hii kwa kutupatia mnara katika Kata ya Tandangongoro. Tandangongoro sasa inazungumza; je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika Jimbo la Lindi, hususan katika maeneo ya Kata ya Chikonji, Kitumbikwela, Mbanja na Rasbura?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Lindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yetu tunatekeleza mpango wa miaka mitano wa kujenga minara katika mikoa na wilaya zote nchini ikiwemo Jimbo la Lindi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wetu huu tutafika katika jimbo lake na tutafanya kama anavyoomba kujenga minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* kutuma wataalamu katika jimbo hili kufanya tathmini ya uhitaji wa minara katika jimbo lake ili tuingize katika mpango wetu wa miaka mitano wa ujenzi wa minara nchi nzima. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na changamoto sana ya mtandao maeneo ya Kiumba, Kata ya Lyamkena Jimbo la Makambako lakini hali kadhalika Kata ya Ilembula Jimbo la Wanging'ombe kwenye baadhi ya vijiji kikiwemo na Igula.

Je, ni lini mtahakikisha kwamba mnaimarisha kwa kuweka minara ambayo wananchi hao waweze kupata mawasiliano vizuri bila usumbufu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Njombe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* kwenda katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na Mkoa wa Njombe kufanya tathmini ya changamoto ya mawasiliano katika kata alizozitaja ili tutambue changamoto iliyopo na kupata namna bora ya kulitatua. Kama ni ujenzi wa minara mipya au kama ni kuongezea nguvu minara iliyopo basi tufahamu tutatumia njia gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutakwenda katika jimbo lake na mkoa wake kufanya tathmini na pale tutakapogundua udhaifu tutarekebisha, kama ni ujenzi wa minara mipya tutajenga na kama ni kuongeza nguvu tutaongeza nguvu na katika mpango wetu wa miaka mitano tutahakikisha kwamba ifikapo mwaka 2030 changamoto ya mawasiliano nchini tutakuwa tumeitatua kwa kiwango kikubwa kama siyo kuimaliza kabisa. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Switbert Mkama, Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa ni Wizara ya Maji. Ninamwita Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, Mbunge wa Sikonge, aweze kuuliza swali lake.

Na. 503

**Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria - Sikonge**

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA** aliuliza: -

Je, lini maji ya Ziwa Victoria yataanza kusambazwa katika Kata za Pangale, Mpombwe, Igigwa, Kisanga, Tutuo, Mkolye, Chabutwa na Ipoje?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Amosy William Maganga, Mbunge wa Jimbo la Sikonge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28 kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria

kutoka Tabora kwenda katika Wilaya za Sikonge, Urambo na Kaliua mkoani Tabora kwa gharama ya shilingi bilioni 143.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 253 sambamba na ujenzi wa matanki tano yenye jumla ya ujazo wa lita milioni nane yakiwemo matanki mawili yenye ujazo wa lita milioni tatu yaliyojengwa katika maeneo ya Tumbili na Misheni, wilayani Sikonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo umefikia wastani wa 76.5% za utekelezaji na umeanza kutoa huduma kwenye baadhi ya maeneo ya Mji wa Sikonge wakati utekelezaji ukiendelea. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2026 ambapo Serikali itafanya usanifu wa kufikisha huduma ya maji kupitia mradi huo kwenye maeneo ya pembezoni umbali wa kilometa 12 kutoka bomba kuu ikiwemo Kata za Pangale, Mpombwe, Igigwa, Kisanga, Tutuo, Mkolye, Chabutwa na Ipoje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga, maswali ya nyongeza.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi na vilevile nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pamoja na majibu hayo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwa vile tanki la maji katika Kijiji cha Tumbili, Kata ya Igigwa tayari limeshajengwa na kwa vile tanki hili tayari limeshajazwa maji takribani miezi miwili iliyopita kwa ajili ya kusambaza maji kwenye kata hizo za Igigwa, Pangale, Ipole, Tutuo pamoja na Mole.

Je, Mheshimiwa Waziri sasa haoni kwamba wakati umefika kwamba hayo maji ambayo tayari yameshajazwa yaanze kusambazwa kwa wananchi hawa ili kuwaondolea adha kubwa ya ukosefu wa maji waliyonayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Kata ya Kilumbi pamoja na Kata ya Kipili wana adha kubwa, wana changamoto kubwa sana ya maji, na suluhu ya kata hizo ni ujenzi wa Bwawa la Kilumbi.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka wataalamu wake ili waweze kufanya tathmini na hatimaye kuanza ujenzi wa bwawa hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Amosy William Maganga, Mbunge wa Sikonge kwa namna ambavyo ameingia na kuhakikisha kwamba anasukuma sana huduma ya maji katika Mji wa Sikonge na kwa namna ambavyo anaendelea kutushirikisha Wizara ya Maji na katika *package* hii ya Urambo, Kaliua pamoja na Sikonge ni Sikonge pekee ndiyo imekuwa ya kwanza kuhakikisha kwamba maji yanaanza kutoa huduma kwa wananchi kama ambavyo nimesema katika jibu langu la msingi. Hii ni kwa sababu ya msukumo wake ambao anaendelea kutupa ushirikiano sisi Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tanki la Tumbili ni kweli kabisa kwamba tulilijaza maji na Mheshimiwa Waziri alifika Sikonge kwa ajili ya kufanya *testing* ya yale maji katika lile tanki. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba baada ya kufanya *test* na kukamilika tutaanza sasa kusambaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi ni kwamba tuhakikishe ile miundobinu hakuna maji yatakuwa yanavuja ambayo yatasababisha kupoteza maji. Kwa hiyo, ndiyo maana bado tuko katika hatua za mwisho na baada ya hapo tutaanza mara moja kuhakikisha kwamba watu wako wa Sikonge wanasambaziwa maji ikiwemo kilometa 12 katika maeneo ya pembezoni ambayo Mheshimiwa Rais ameelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili Kata ya Kilumbi; hii ni kata ambayo iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2025/2030 na hivyo bwawa ndiyo suluhisho. Nimtoe

hofu, Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni sikivu sana na kwa sababu amesema na sisi tutatuma timu yetu kwenda kufanya *need assessment.* Baada ya hapo tufanye *feasibility study* na baada ya hapo tufanye usanifu wa kina. Baada ya hapo tupate fedha kwa ajili ya kujenga bwawa kwa ajili ya wananchi wake wa Kata ya Kilumbi pamoja na Kata ya Kipili. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri ndani ya Jimbo la Segerea kwa mujibu wa ratiba ya *DAWASA* tunapata maji kwa mgao na huo mgao kwa sasa ndani ya Jimbo la Segerea umebaki katika makaratasi ya ratiba. Wananchi wa Jimbo la Segerea hawapati maji hata kwa huo mgao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi ambao mpaka sasa ni miezi 10, ni mwaka mmoja, ni miezi sita, ni mitatu hawapati maji safi na salama ya mgao na Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo kwamba wananchi wa Segerea wapate maji kulingana na ratiba ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kufahamu, nini kauli ya Serikali leo kwa jambo hili ambalo wananchi wanaambiwa mnapata maji, lakini maji hawapati. Ninapenda nisikie kauli ya Serikali kwa wananchi wangu wa Jimbo la Segerea. Ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba swali hili aliliuliza wiki iliyopita, lakini ameliuliza kwa namna tofauti kwa leo,

lakini mantiki yake iko pale pale kwamba anahitaji wananchi wake wa Segerea wapate maji ya uhakika ambayo pia ratiba ya mgao iweze kutabirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo ni katika suala lile lile la kuhakikisha kwamba pampu zetu zinapopata hitilafu ni lazima tufanye *replacement* ili kuweza kuwa na mnyororo ambao unatambulika, lakini, nitoe maelekezo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa Mtendaji Mkuu wa *DAWASA;* suala la Segerea, wananchi wa Segerea hawahitaji ratiba ambazo hazitabiriki. Wananchi wa Segerea wanahitaji kuona kwamba Serikali yao inawajali, wananchi wa Segerea hawahitaji kuona kila siku Mbunge wao anapiga kelele kuhusu Segerea, wananchi wa Segerea tutahakikisha kwamba baada ya kutoa maelekezo haya tunahitaji kuona matokeo na Mkurugenzi wa *DAWASA* alifanyie kazi kwa ukaribu sana jambo hili ili isiwe kama wimbo wa Taifa katika kutatua changamoto za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa maelekezo tusizoee changamoto za wananchi, tuchukue hatua na tuweze kuona matokeo na wananchi wa Segerea wapate huduma ya uhakika na hata kama kuna mgao basi mgao huo uwe na taarifa maalum, lakini pia uweze kutabirika. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitakaowapa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, ili tuweze kupata wengi tafadhali yawe mafupi na yaendane na swali la msingi.

Mheshimiwa Christina Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa Serikali imekuwa ikitekeleza kwa vitendo Sera ya Maji ikiwemo usambazaji wa maji kutoka Ziwa Victoria na kufikisha maeneo ambayo kuna uhitaji, tunaipongeza Serikali na kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kutuletea mradi wa maji wa Ziwa Victoria, Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa bado kuna maeneo mengi Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria bado haujakamilika na hivyo wanawake na wasichana kuendelea kupata shida ya kutafuta maji umbali mrefu.

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria utakamilika katika Kata za Kigwa, Goweko, Igalula na Nsololo ili kuwaondolea wananchi adha ya ukosefu wa maji safi na salama katika Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Christina Mndeme, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Tabora na kwa kumbukumbu yangu inaonesha kwamba katika sekta yetu ya maji leo inawezekana ikawa mara ya tano kuulizia masuala ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa na ni ishara tosha kwamba amedhamiria kuwapambania Wana-Tabora hasa wakina mama ambao wamemtuma kuingia Bungeni na kuwa sauti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, Serikali kupitia Wizara ya Maji tutaendelea kukupatia ushirikiano na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya uwekezaji mkubwa wa shilingi bilioni 680 kutoka Ihelele kuja mpaka Tabora na sasa shilingi bilioni 143 kutoka Tabora kwenda Sikonge, Kaliua pamoja na Urambo na huu upande wa Igalula ambapo kuna Goweko, kuna Kigwa na kuna Nsololo. Mradi huo hivi sasa tayari tumeshashusha mabomba ya kutosha ili tuanze usambazaji wa wananchi wa Igalula, Kigwa pamoja na Nsololo. Lengo ni moja tu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kwa vitendo kumtua mama ndio kichwani. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Exaud Kigahe.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mufindi Kaskazini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa miradi mingi sana ikiwemo mradi wa maji wa kata tatu: Kata za Ihalimba, Ifwagi na Ikongosi. Mradi huu ni wa kihistoria, lakini umesimama kidogo kwa sababu mkandarasi hajapata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itampa fedha ili mkandarasi aweze kukamilisha mradi huu wa kihistoria ikiwa ni azma ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kumtua mama ndoo kichwani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, kama ambavyo amesema kuwa kuna mradi huo mkubwa. Wiki moja iliyopita tulikuwa na ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ndani ya Jimbo la Mheshimiwa Exaud Silaoneka, lakini pia mradi huu ambao ni uwekezaji mkubwa sana una gharama ya shilingi bilioni 41. Gharama hii ni uwekezaji mkubwa sana kuwahi kutokea katika Jimbo la Mufindi Kaskazini ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka, lakini pia ni kutokana na ushawishi wake na ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa ahadi ya Serikali, ahadi ile ambayo tuliitoa mbele ya Waziri Mkuu iko palepale na utekelezaji wa kuhakikisha kwamba tunasukuma pesa kupeleka upo pale pale. Ninamuomba avute Subira, wakati tunamalizia hatua za mwishoni kum-*engage* mkandarasi ili aweze kuendelea na mradi huo, ninaamini kwamba ndani ya muda mfupi mkandarasi atarudi na kuendelea na mradi huo. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba niipongeze Serikali na kukupongeza wewe mwenyewe Waziri, uli-*sign* Mradi wa Ng'ang'ange na tumepatiwa pesa. Je, ni lini sasa Mradi wa Kihesa Mgagao ambao tayari 85% mkandarasi ameshatekeleza utapatiwa pesa ili wananchi waweze kupata maji safi na salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa kutambua na kwa kuleta mrejesho. Alikuwa na anaongelea Ng'ang'ange kila siku akisimama hapa bungeni na Mheshimiwa Rais amepeleka fedha ndani ya mradi ule na tayari Mheshimiwa Kabati amepata matumaini ya kwamba Serikali hii inasema na kutenda na wananchi wasubiri matokeo ya kuona maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe hofu, katika huu mradi ambao umefikia 80% na kitu nimtoe hofu. Kwa staili hiyo hiyo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kusema na kutenda nakuhakikishia hilo nalo tutalifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Kilolo waendelee kufurahia huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kija Ntemi, swali la nyongeza.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri kwanza nikupongeze kwa majibu mazuri unavyoendelea kutujibu; lakini Mheshimiwa Waziri katika Jimbo la Katoro ni kweli umetuletea maji lakini changamoto maji yanakatika sana, wakati mwingi maji hayapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofika wakati wa kusoma mita kwamba tulipe sasa maji ndipo maji yanaweza kutoka siku mbili ili watu waweze kulipa zile bili.

Mheshimiwa Waziri, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba Wananchi wa Katoro wanapata maji wakati wote kwa sababu Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewekeza fedha nyingi ili wananchi wale waweze kupata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate uhakika wa wananchi wa Katoro kuweza kupata maji kila siku au kuna changamoto gani ambayo inasababisha maji yanakatika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kija Ntemi, Mbunge wa Katoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kumshukuru sana, yuko Bungeni, lakini anajua kinachotokea ndani ya jimbo lake, hii ni kuonesha kwamba ametumwa kufanya kazi ya wananchi na wananchi wanaona matokeo ya kumchagua. Nakupongeza sana na hii niitumie kama fursa ya kupata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge ili sasa Serikali twende tukafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji namwelekeza *Regional Manager* wa *RUWASA* Mkoa wa Geita aende Katoro akafanyie kazi hiyo changamoto. Tujiridhishe changamoto ni nini, kama ni upungufu wa maji ama ni changamoto ya umeme. Baada ya hapo tutajua tunachukua hatua gani ili mradi tu wananchi wa Katoro wawe na uhakika wa kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Regina Malima, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kwa niaba ya vyuo na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuna changamoto ya baadhi ya vyuo vilivyoko kando kando ya Ziwa Victoria, lakini pia shule za sekondari *especially* kwenye Majimbo ya Mwibara na hata Jimbo la Ukerewe.

Je, Serikali iko tayari kufanya uhakiki wa shule hizo na zenyewe kuingia katika mpango wa huu Mradi wa Ziwa Victoria? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Regina kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la msingi sana ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliongelea na kwa sababu Watanzania wote kwa mujibu wa Sera yetu ya Maji ya mwaka 2002 Toleo la mwaka 2025 ni kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma ya maji safi na salama hususan katika maeneo haya ya chuo, tutakaa na wenzetu Wizara ya Sayansi na Elimu ya Juu lakini pia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, kwa upande wa shule za sekondari na msingi ili tuweke mkakati wa pamoja namna ya kwenda kushughulika na changamoto zilizoko katika vyuo, sekondari pamoja na shule za msingi. Lengo ni kutimiza azma ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anakuwa na *access* ya maji safi na salama. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, swali la nyongeza.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri kwamba siku chache zilizopita baada ya kuhoji hapa juu ya malipo ya mkandarasi Tunduru Mjini katika mradi wa usambazaji wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 3.4, naomba nikiri kwamba Serikali *promptly* imetekeleza na imemlipa mkandarasi yule. Kwa hiyo napenda kutambua jitihada hizo na kuipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kufahamu ni lini mradi ule wa usambazaji wa maji Tunduru Mjini utakamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ado Shaibu, Mbunge, na kwa hakika Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshajipambanua na kuhakikisha kwamba maendeleo hayana chama na ndiyo maana tunashuhudia kwamba Mheshimiwa Mbunge kaomba na Serikali imechukua hatua. Maana yake wananchi wa Mheshimiwa Ado Shaibu wanaendelea kushuhudia utekelezaji mzuri kabisa wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi ukiwa unatekelezwa na Mheshimiwa Ado Shaibu katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba yeye kama sauti ya wananchi wake tutaendelea kumpatia ushirikiano hasa katika jambo ambalo amelisema la kusogeza huduma zaidi kwenye makazi ya wananchi kupitia usambazaji wa mabomba. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo siku ile nilikujibu na Serikali imetenda, hili nalo nakujibu nikiwa nakupatia matumaini ya kutosha kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kumtua mama ndio kichwani hana mchezo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhani Singano, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuendeleza vyanzo vya Mandui, Maao, Makangha na Kweusolo Kata ya Mahezangulu, Bumbuli kwa ajili ya kuongeza huduma ya maji katika kata hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhani Singano, Mbunge mahiri kabisa kutoka pale Bumbuli na kwa kazi kubwa akiwa pia ni sehemu ya washauri wa sekta ya maji akiwa Mjumbe wa Kamati ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, Serikali imejizatiti na imejipanga na nikuombe Mheshimiwa Mbunge endelea kushirikiana nasi katika hili ili tuhakikishe kwamba tunaenda kuviendeleza vyanzo hivi ili viweze kuendelea kutoa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninaomba nitumie fursa hii kumuomba Mheshimiwa Mbunge baada ya Vikao vya Bunge kumalizika tukae, bado uhitaji wake, ujuzi wake na ufundi wake tunauhitaji katika kushauri ili tuone njia bora zaidi ya kwenda kutekeleza hili ambalo ameliomba. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haiderali Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Itaja, Kijiji cha Gairo wananchi hawana maji. Kila kukicha wanaingia gharama kununua maji. Serikali inatuhakikishia vipi kwamba tatizo hilo sasa litakomeshwa na wananchi wetu Kata ya Itaja, Kijiji cha Gairo, Jimbo la Ilongero watapata maji?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua mahitaji ya Watanzania na wananchi wote ni kuweza kupata huduma ya maji safi na salama, lakini pia tunatambua katika vijiji 12,333 kazi kubwa imeshafanyika na sasa tumebaki na vijiji 1,575.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi tumevigawanya kwa awamu ambapo kila mwaka tutaanza kutekeleza vijiji 300. Kwa hiyo, tunaamini ndani ya kipindi cha miaka mitano, kikiwemo kijiji cha Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kutekeleza, kwa sababu siyo kijiji kimoja tu. Tunafahamu kwamba hata kwenye jimbo lake siyo kijiji kimoja vipo vingi ambavyo bado havijapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza kutekeleza awamu kwa awamu, tukianzia mwaka wa fedha 2026/2027 tutatekeleza vijiji 300. Mwaka ujao tutatekeleza vijiji 300 mpaka itakapofika mwaka 2030 tutakuwa tumekamilisha vijiji 1,575 maana yake vijiji vyote Tanzania vitakuwa vimepata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nancy Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kata ya Mahenge katika Wilaya ya Kilolo ni kata ambayo haijawahi kupata maji ya bomba na chanzo tayari kimeshapatikana. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji katika kata hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijalisikia swali vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nancy Nyalusi, tafadhali rudia swali lako.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mahenge katika Jimbo la Kilolo, Wilaya ya Kilolo ni kata ambayo haijawahi kupata maji ya bomba tangu kuanzishwa kwake. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa ili kuanza ujenzi wa mradi wa maji katika kata hiyo kwa sababu chanzo tayari kimeshapatikana?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge na amekuwa akiwasemea akina mama wa Mkoa wa Iringa hasa tukiwa pia kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimtoe hofu, katika Jimbo hili la Kilolo na katika hii kata nakuhakikishia kwamba Mheshimiwa Rais alishasema hakuna kijiji, hakuna mtaa, hakuna kata ambayo itaachwa nyuma kwenye kuhakikisha kwamba tunaileteа huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo ni mpango, na kupanga ni kuchagua. Tunapanga hatua kwa hatua na hakuna uwezekano wa kuanzisha miradi yote kwa pamoja na ikaisha kwa pamoja. Ninachotaka kusema, kipaumbele chetu kwa sasa miradi ambayo imeshaanza tunahitaji tuikamilishe na iweze kutoa matokeo na baada ya hapo tutapanga kwa ajili ya miradi ambayo haijaanza ili wananchi...

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ya Watanzania ni lini? Nikutoe hofu, kuanzia sasa mpaka mwaka 2030 eneo la kata hiyo litakuwa limepata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba namwita Mheshimiwa Kangi Lugola.

Na. 504

**Pesa za Miradi Tisa ya Maji - Bunda Mjini**

**MHE. KANGI A. LUGOLA K.n.y. MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha zilizobaki za utekelezaji wa miradi tisa ya maji yenye thamani ya shilingi bilioni 13 ambapo zimetolewa shilingi bilioni saba tu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi nane katika Jimbo la Bunda Mjini, Mkoani Mara kwa gharama ya jumla ya shilingi 21,671,846,983.12 ambapo hadi kufikia sasa jumla ya shilingi bilioni 13.7 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kwa hati ya madai zinazowasilishwa na kadri fedha zinavyopatikana ili iweze kukamilika kwa wakati na ubora stahiki. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola, maswali ya nyongeza.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia kwa kutupatia shilingi bilioni saba Wananchi wa Bunda Mjini ili miradi hiyo iweze kukamilika. Pamoja na hayo Wananchi wa Bunda Mjini

wanategemea mradi mmoja tu wa Nyabehu ambao ndiyo unawapatia maji, lakini kwa miezi ya hivi karibuni kumekuwa na upotevu wa maji kwa mabomba kupasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni haja ya kuchukua hatua za haraka kupeleka fedha ili kuweza kudhibiti upoteaji wa maji ili Wananchi wa Bunda Mjini wapate maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Vijiji vya Sikiro, Mugara, Nyarugoma, Isanju, Mwiruruma na Muhula, Muranda, Chingurubira pamoja na Karukekere vinategemea Mradi wa Maji wa Isanju ambao kwa miezi minne sasa pampu ilikuwa imeharibika. Hata hivyo, taarifa tulizonazo ni kwamba pampu hii ilishakuja zaidi ya miezi miwili. Sasa kama hii pampu siyo pampu hewa ni sababu gani zinasababisha pampu hiyo isifungwe ili wananchi hawa waweze kupata maji? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ambayo yameulizwa na Mbunge wa Mwibara, Mheshimiwa Kangi Lugola, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua umuhimu wa kukamilisha miradi ya maji nchini na kwa vile kukamilisha miradi ya maji nchini siyo mafanikio ya Serikali pekee bali ni ushindi kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatambua umuhimu huo, lakini pia mradi huu ambao Mheshimiwa Mbunge ameuongelea kuhusu upotevu wa maji kwa sababu ya mabomba kupasuka, nimtoe hofu, mradi huu tayari tumeshaanza kuurekebisha, mabomba ya zamani yaliyokuwa yanafanya kazi pale yalikuwa *GRP* sasa tumeyabadilisha na sasa tunaweka *steel pipes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimepata picha ya kuonesha tayari kuna kilometa 2.1 tayari wameshayabadilisha hayo

mabomba na tunaendelea na kilometa nyingine ambazo ni zaidi ya kama kilometa nne hivi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kwa kasi ambayo wanaenda nayo ndani ya muda mfupi bomba hilo litakuwa limerekebishwa na upotevu wa maji hautokuwepo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaendelea kuboresha taasisi zetu na usimamizi wa wataalamu wetu. Mheshimiwa Waziri wa Maji jana amefanya marekebisho na kufanya maboresho katika utendaji wa sekta yetu ya maji ikiwemo Bunda Mjini pamoja na maeneo mengine. Lengo ni kuhakikisha kuongeza tija katika utendaji wao na kuhakikisha kwamba wanachukua hatua za haraka tatizo linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pampu ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliongelea, sioni sababu pampu iwe imenunuliwa miezi miwili na ikawa bado haijafungwa na mtendaji wetu yuko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoa maelekezo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninataka ndani ya wiki hii kama hakuna *any technical problem* zingine ambazo zinaambatana na uwepo wa ile pampu, basi pampu hiyo iwe imeshafungwa na vijiji vitano vya Mheshimiwa Mbunge waendelee kupata huduma ya maji safi na salama. Kinyume cha hapo tutachukua hatua kali zaidi kuhakikisha kwamba watendaji wanaendelea kujirekebisha na kuchukua hatua pale tatizo linapokuwa linajitokeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kutokana na changamoto ya kupasuka kwa mabomba, changamoto ambayo inasababisha upotevu wa maji, Serikali inaonaje ikaanzisha namba maalumu ya kuripoti changamoto hiyo? Kwa sababu mara nyingi mimi nimekuta maji yanamwagika na ukiuliza wahusika wanasema hawajui mahali pa kuripoti. La kwangu ni hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa unaweza ukarudia swali lako na Waheshimiwa Wabunge tunaomba tupunguze sauti ili muuliza swali na mjibu swali waweze kusikilizana.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto ya kupasuka kwa mabomba, changamoto ambayo inapelekea upotevu wa maji, Serikali inaonaje ikaanzisha namba maalumu kwa ajili ya kuripoti changamoto hiyo inapotokea? Kwa sababu kuna maeneo ukipita ukakuta maji yanamwagika kutokana na kwamba bomba limepasuka ukiuliza wahusika wanasema kwamba hawajui wanaripoti wapi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali muhimu sana na linajenga msingi imara wa ushirikishwaji wa wananchi pale wanapoona kuna miundombinu imepata changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tayari tuna hizo namba isipokuwa naona kwamba tutabadilisha namna ya kuhakikisha kwamba namba hizi zinafahamika kwa wananchi. Lengo ni kwamba tuweze kushirikiana kutoa taarifa pale ambapo mabomba yanakuwa yamepasuka na kuweza kuokoa maji yanayopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea ushauri wa Mheshimiwa Stella na kwa umuhimu wake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Jimbo la Bunda kuna Mradi wa Nyamuswa una shilingi bilioni nane, umekwama hauendelei; Mradi wa Hunyari shilingi milioni 830, umekwama hauendelei; na Mradi wa Lambo la Mihingo shilingi bilioni 1.5 umekwama

hauendelei. Ni lini sasa Waziri tutakaa na wewe na wakuu wa *RUWASA* wa mkoa na wilaya tujadili miradi ya Jimbo la Bunda?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Getere ameomba ni lini tutakaa na viongozi wa wilaya na mkoa. Sisi tuko tayari dakika yoyote na Wizara itakupatia ushirikiano pale ambapo tutakaa na kupanga tarehe maalumu na kufanya mwaliko ili wahusika ambao umewataja tuweze kukaa nao kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunatambua kuna utekelezaji wa miradi ndani ya Jimbo la Bunda, lakini sambamba na hilo tunafahamu kwamba kuna uhitaji wa fedha ikiwemo Mradi wa Nyamuswa ambapo na mimi niliweza kufika katika mradi huo naufahamu vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, juzi hapa Wizara ya Maji tumepeleka kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya miradi hiyo hiyo ambayo inaendelea kutekelezwa ndani ya Jimbo la Bunda. Nikutoe hofu, sambamba na kikao ambacho umekiomba Serikali bado itaendelea kufanya juhudi za haraka sana kuendelea kuhakikisha kwamba tunawafikishia huduma ya maji safi na salama kwa kupeleka fedha katika miradi inayoendelea ili iweze kukamilika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 505

**Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Tsoray – Mbulu**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Tsoray utakaohudumia vijiji 21 katika Halmashuri ya Mji wa Mbulu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha zaidi ya shilingi bilioni 70 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Kimkakati wa Tsoray uliopo Tarafa ya Nambis, Wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji chenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 13.6 kwa siku, ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house)*, ununuzi na ufungaji wa pampu nne za kusukuma maji, ujenzi wa matanki nane yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 6.6, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 429.5, ujenzi wa vituo 160 vya kuchotea maji sambamba na ujenzi wa mbauti *(cattle trough)* sita za kunyweshea mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo ukianza kutekelezwa unatarajiwa kuchukuwa miezi 24 ambapo unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 109,228 waishio kwenye vijiji 21 vya Wilaya ya Mbulu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kuleta mradi mkubwa na wa kimkakati unaogharimu shilingi bilioni 70.1 katika Tarafa ya Nambis na katika Jimbo la Mbulu Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mradi huu fedha ikipatikana utatekelezwa ndani ya miezi 24. Sasa kwa bahati nzuri chanzo cha maji katika mradi huu ni Mto Tsoray ambao unapitisha maji mwaka mzima. Sasa ni upi mkakati wa Serikali wa kuwasaidia wale ambao angalau wako kwenye chanzo cha maji kuendelea kupata maji safi na salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri, je, uko tayari kuambatana na mimi kwenda kutembelea Tarafa ya Nambis kujionea changamoto kubwa ya maji iliyoko hapo na kuwatia moyo wale wananchi kwa kuwa wanausubiri mradi huu kwa hamu kubwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza, na kwa faida ya *Hansard*, hili swali uliliuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Mjini na kwamba sambamba na hilo pia, ninapenda kujibu maswali ya Serikali kwa mtazamo ule ule ambao niliujibu siku ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kutafuta fedha shilingi bilioni 70 zipatikane kwa pamoja, ninafikiri itakuwa ni suala ambalo ambalo litachukua muda zaidi na tukakubaliana kwamba mradi huu tutaanza kuutekeleza kwa awamu ili angalau tunapoenda kupata zile fedha zingine basi tunakuja kutumia kama kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema kwamba kutokana na ule Mto wa Tsoray, lakini pia tuna uwezo wa kujenga kwanza tanki, *treatment plant* (mtambo wa kutibu maji) ili wananchi waanze kupitia *existing infrastructure* kupata huduma ya maji

wakati Serikali ikiwa inatafuta fedha za kujenga miundobinu mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge dada yangu Mheshimiwa Yustina katika ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akiuongelea sana huu mradi, lakini pia na maeneo mengine ya Mkoa mzima wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba anayo kiu kubwa ya kuona akina mama hawaachi shughuli za kiuchumi kwenda kutafuta maji. Ninamtoa hofu, mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, niko tayari kuongozana naye katika maeneo ambayo ameyataja ili tukajionea hali halisi ya huduma ya maji na baada ya hapo, tufanye tathmini na kuchukua hatua kulingana na mahitaji ambayo yatakuwa yamebainika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Pius Yanda, swali la nyongeza.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Rusaba hawajawahi kufaidika na huduma ya maji safi na salama. Sasa ninaomba kufahamu ni lini wananchi hao watawezeshwa kupata maji safi na salama katika kata hiyo katika Wilaya ya Buhigwe?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Pius Yanda, Mbunge wa Jimbo la Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwanza kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Pius Yanda kwa kuwatetea Wana-Buhigwe na vilevile kuitetea sekta ya maji, yeye akiwa kama mtafiti katika vyanzo vya maji, ameisaidia sana Serikali hii na sasa

ndiyo Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na Mazingira, anatambua umuhimu mkubwa sana wa kuwa na maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, hili tunalichukua kwa uzito kwa kufuata falsafa ile ile ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba wananchi wa kata hiyo ni lazima tukawatue akina mama ndoo kichwani. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakar Omari, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKAR A. OMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wa maeneo ya Jimbo la Manonga ambao wameshafikiwa na mradi wa maji ya Ziwa Victoria, lakini upatikanaji wake imekuwa ni matatizo makubwa sana. Inapita mpaka wiki mbili, tatu maji haijatoka. Kuna shule ya sekondari iko Ntigu maeneo ya Ntigu, Usongo, wanafunzi imebidi waondoke kwa kukosa maji.

Je, Serikali ina mipango gani wa kuhakikisha maji ambayo yamekuja kwa gharama kubwa sana ya Serikali na yanapatikana kwa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakar Omari tafadhali rudia swali lako na isogelee *microphone*. Sogelea kipaza sauti Mheshimiwa.

**MHE. ABUBAKAR A. OMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi; wananchi wangu wa Jimbo la Manonga maeneo ambayo Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria yamefika, lakini maji hayatoki mpaka wiki mbili mpaka tatu kiasi kwamba watu sasa hivi ukiwatajia Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria maeneo yale, wanakuwa yaani hawakuelewi. Kwa mfano, sasa hivi kuna wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Seif Gulamali wameanza

kuondoka shuleni kwa kukosa maji wiki ya pili mpaka tatu sasa hivi. Shida ni nini hasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abubakar; jambo ambalo ameliongea ni jambo ambalo ni zito kidogo na ni la msingi sana. Wananchi ama wanafunzi kutoka shuleni ama kuondoka shuleni kwa sababu ya kukosa huduma ya maji safi na salama, si utaratibu na wala siyo maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Baada ya kikao hiki cha Bunge Mheshimiwa Mbunge tuonane ili tuende kuhakikisha kwamba tunachukua hatua za haraka ili wananchi na wanafunzi wa shule hiyo wanapata huduma ambayo inatarajiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo, Naibu Waziri wa Maji, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea, sasa ni Wizara ya Ujenzi. Ninamwita Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Missenyi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 506

**Ujenzi wa Barabara ya Katoma – Bukwali**

**MHE. FROLENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga bajeti ya kutosha ili kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Katoma – Bukwali badala ya kujenga mita 200 kila mwaka?

**MWENYEKITI:** Majibu, Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Missenyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala ya Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea na ujenzi wa Barabara ya Katoma – Bukwali kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 8.2 kati ya kilometa 39.83 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu iliyobaki kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea na imefikia 65%. Baada ya usanifu kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi kwa ajili ya maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapongeza juhudi za Serikali kwenye Barabara hii ya Katoma – Bukwali ambayo imeendelea kutengenezwa kwa kiwango ambacho inapitika hadi sasa, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ninaendelea kuipongeza Wizara ya Ujenzi chini ya Mheshimiwa Ulega ambaye amekuwa ni mhimili katika ujenzi wa barabara na Wilaya ya Missenyi inaendelea kufaidi usimamizi wako, lakini pia kuwepo kwa Meneja wetu wa Mkoa *Engineer* Joel, ameendelea kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo kwa sasa imejengwa kilometa 8.2 kwa miaka 10 ambapo imekuwa ikijengwa meta 200; 200. Sasa ni nini ji jibu lenye matumaini kwa Wananchi wa Missenyi kwamba barabara hiyo kilometa 31 lilizobaki zitakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Ulega amekuwa ni mwanajamii wa Missenyi na anajua wazee wangu

wa Missenyi akina Sheikh wa Mkoa Alhaj Haruna Abdallah Kichwabuta, Mlangira Justin Lambert Kaiza, Ruimbao, wote umekuwa nao na barabara umeenda mpaka Bugandika pale. Sasa wazee wangu pale Bugandika – Kitobo – Buyango mpaka Ruzinga barabara yao kilometa 18 tu wanasema kijana wetu tupeleke kwa Mheshimiwa Waziri wetu.

Je, ni lini na sasa barabara hiyo ya Mshenye – Bugandika – Kitobo – Uyango mpaka Ruzinga itajengwa kwa kiwango cha lami ili na wazee hao angalau wasipite kwenye barabara ambayo ina mashimo mengi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Missenyi *Comrade Kyombo* na ninampongeza kwa umahiri wake na ufuatiliaji wa karibu sana wa hoja za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hili la kuchukua muda mrefu wa Barabara ya Katoma – Bukwali, ninakiri kwamba tunakwenda kukamilisha upembuzi yakinifu wa sehemu iliyobaki. Sehemu ambayo tunakwenda ukamilifu wake kufika mwezi Septemba mwaka huu, mkandarasi anayefanya kazi ya upembuzi yakinifu atakuwa amekamilisha, na baada ya kupata uhakika wa gharama, sasa tutakwenda kuitangaza barabara hii yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu mradi huu ni miongoni mwa miradi inayoendelea, na ni msisitizo wa Serikali katika *commitment* ya Serikali ni kwamba tutahakikisha miradi yote inayoendelea na miradi yote iliyosainiwa, ndiyo kipaumbele chetu. Sasa mradi huu wa Bukwali kutokea Katoma ni miongoni mwa miradi hiyo na kwa msingi huo, wewe na Wana-Missenyi wote waendelee kuwa na subira, tutafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hivi sasa tumeendelea kufanya ubunifu kwa vyanzo vya mapato ya kuhakikisha kwamba miradi yetu hii yote ambayo inaendelea na

iliyosainiwa iwe na vyanzo vya uhakika ili wakandarasi waweze kurudi *site* na waendeleze kazi ya kujenga miundobinu ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hizo, tunavyo vyanzo vya *PPP*, tunacho chanzo cha uhakika cha Mfuko wa Barabara ambacho kitakwenda kufanya vizuri na ninawahakikishia Wabunge wote kwa kuwa mmetoa maoni na nina hakika Serikali imeyapokea, na vyanzo vya kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina na hiyo itapelekea kuijenga barabara ile. Miji ya Kanyigo na mingine, yote itapata siyo tu kujengewa lami, lakini na kuwekewa taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lake la pili Mheshimiwa Kyombo ni Barabara za Missenyi na amewataja baadhi ya wazee wetu wa kule Kagera akiwemo Sheikh Kichwabuta na Kaka yangu Lambert ambao barabara zao na mimi ni kweli nimepita huko mara kadhaa nikienda katika shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kushiriki misiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukua hoja hii na kwenda kuifanyia kazi, ninamwagiza Meneja wa Mkoa wa Kagera ahakikishe ya kwamba anakwenda kuziweka katika kipaumbele barabara hizi ili tuweze kuzifanyia kazi na hatimaye tuweze kutoa huduma iliyo nzuri kwa wananchi wa maeneo haya. Hongera sana Mheshimiwa Kyombo kwa ufuatiliaji mzuri wa shughuli na maendeleo ya Wananchi wa Missenyi, lakini na Mkoa mzima wa Kagera. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Barabara ya Makofia – Mlandizi – Mzenga ina hali mbaya kutokana na mvua hizi zilizonyesha.

Je, Serikali ina mpango gani wa matengenezo ya dharura ili kuwaondolea shida Wananchi wa Bagamoyo ambao kwa sasa usafiri kuanzia jioni haupatikani na hata pikipiki bei imepanda mpaka shilingi 10,000 wakati wanasubiria ahadi ya Serikali ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Bagamoyo, Dada yangu Subira Mgalu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Barabara ya Makofia inayopita katika Miji ya Yombo, Viswe mpaka unafika Mlandizi na baadaye kutoka Mlandizi kwenda Mzenga, ni barabara ya kimkakati na ni barabara muhimu sana kwenye kuhakikisha pia inakuwa ni mbadala wa Barabara Kuu ya Morogoro kwa maana ya Kibaha - Chalinze mpaka Morogoro, na kwa hiyo, barabara hii inapokuwa katika hali nzuri, inarahisisha watumiaji hata wanaokwenda katika mikoa mingine wanaotokea Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwagiza Meneja wetu wa Mkoa wa Pwani kuhakikisha kwamba tunakwenda kuifanyia ukarabati, mvua zimekwishakupungua na kuisha kabisa katika maeneo yetu. Kwa hiyo, sasa atoe nafasi kwa mkandarasi kwenda kuisafisha barabara hii ambayo ni ya kimkakati kwenye kupunguza msongamano wa barabara kubwa ya Chalinze mpaka Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Subira Mgalu kwa msisitizo wake na ufuatiliaji wake wa barabara hii hadi kufikia tumeiweka katika mpango wa bajeti ya mwaka 2026/2027 kama barabara ya upunguzaji wa msongamano wa barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutahakikisha kwamba tutaitangaza barabara hii, kupata mkandarasi na hatimaye ili tutakapokuwa tunajenga barabara kuu ya *expressway* ya kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro ambayo ni mkakati wa Serikali

kuifanya kwa njia ya *PPP*, na hivi ninavyozungumza tayari *NSSF* na Kampuni ya *CRJE* wapo kwenye mazungumzo ya mwisho ya kuingia katika kutekeleza mradi huu, basi barabara hii ya Makofia – Mlandizi itakwenda kuwa ni mbadala mzuri wa msongamano wa barabara kubwa ikiwa ni pamoja na barabara ya kutoka *TAMCO* – Mapinga na na kutokea kule Kerege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Barabara ya Mbulu – Garbabi ni barabara aliyopewa mkandarasi wa Kichina kwa miaka minne sasa. Sehemu ya barabara hiyo kutoka Mbulu Mjini kwenda Tlawi ama kwenda pale Tlawi haijatengenezwa kwa miaka minne sasa, mkandarasi huyu wa Kichina anayejenga lami kwa muda mrefu ameshindwa kutengeneza hicho kipande. Mheshimiwa Waziri, nini kauli ya Serikali kumsimamia huyu mkandarasi ili atengeneze hiyo barabara kuondoa adha kubwa sana kwa wananchi wa eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli katika hii barabara tuna mkandarasi huyu aliyekwisha kumtaja na tayari sehemu ya barabara hii wiki mbili zilizopita tumeilipa. Tumelipia fedha ya kuhakikisha kwamba mkandarasi anarudi *site*. Ninafahamu ya kwamba hajarudi *site* bado na moja ya sababu ilikuwa ni hali ya hewa, lakini ninamwagiza sasa mkandarasi na ninamwagiza Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa na *TANROADS* Makao Makuu kuhakikisha kwamba wanamrudisha mkandarasi, anaanza ujenzi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ile sehemu iliyobaki ya kilometa zile 25 ambazo zilikabidhiwa kwa mkandarasi, lakini hazijafanyiwa kazi kwa sababu ya kukosekana kwa fedha ya awali ya malipo kwa mkandarasi yule. Ninamwagiza pia Meneja wa *TANROADS* kwa kuwa barabara hiyo ina mkandarasi wake, lakini hajaanza kazi, bado wajibu huo ni wa kwetu wa kuhakikisha kwamba tunaiboresha ili iweze kupitika wananchi wapate unafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati huu yule anapoanza na wao *TANROADS* mara moja waanze kwa kuisafisha barabara ile ili watu wa Mbulu waweze kupitisha mazao yao ikiwa ni pamoja na mazao ya kilimo kama vile vitunguu na kadhalika kwa urahisi vinavyokwenda sokoni katika Miji ya Arusha, Miji wa Babati na nchini kote kwa ujumla wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory, Mbunge wa Misungwi, aulize swali lake.

Na. 507

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nne Kutoka Kenyatta – Usagara Mwanza**

**MHE. SILVERY L. SALVATORY** aliuliza:

Je, lini upanuzi wa barabara kuu kwa njia nne kutoka Kenyatta – Usagara Mwanza utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa Barabara ya Mwanza Mjini hadi Usagara imekamilika ambapo itahusisha urefu wa kilometa

25 kutoka njia mbili zilizopo sasa kwenda njia nne. Kwa sasa utaratibu wa manunuzi wa kumpata mkandarasi wa ujenzi wa barabara unaendelea. Kazi ya ujenzi itaanza mara moja baada ya mkandarasi kuwa amepatikana, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silvery Salvatory, maswali ya nyongeza.

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa kuna kila dalili ya kwamba mkandarasi amekwishapatikana na wakati wowote ataanza kazi. Je, Serikali iko tayari kuanza upanuzi wa barabara hii kutokea Usagara kuelekea Mjini ukizingatia ukweli kwamba eneo la Usagara halihitaji uhamishaji wa miundombinu kama vile mabomba na taa za barabarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa upanuzi wa barabara hii unaenda kufungua shughuli za kiuchumi. Je, Serikali iko tayari kuanza mchakato wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami; Barabara ya Fulo – Nyambiti hadi Malya yenye urefu wa kilometa 73 kwani barabara hii inauhusiano mkubwa na *dry port* pamoja na *SGR* itakayokuwa kule Fela na itapita kwenye kata yangu ya Fela – Kolomije pamoja Kanyelele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Misungwi, Mheshimiwa Silvery Luboja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana na nimpongeze sana kwa umahiri wake kwenye kufuatilia hoja za

wananchi wa pale Misungwi ambazo ukizitazama zinabeba vilevile eneo lote la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Usagara kwenda Mwanza Mjini ama Mwanza Mjini kuja Usagara kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi la awali, ni kwamba ni barabara ya kimkakati na ni barabara muhimu sana na kwa kweli kwa sasa ni barabara ambayo ina msongamano mkubwa hasa mara baada ya ukamilifu wa Daraja la Kigongo – Busisi kama lilivyotamkwa maarufu Daraja la John Pombe Magufuli. Msongamano umeongezeka sana kwa sababu ni daraja limeleta msisimko mkubwa wa shughuli za kiuchumi katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunatarajia pale Mwanza tutakuwa na kituo kikubwa cha *SGR*, kwa hiyo kitaongeza zaidi ule msongamano wa eneo lile, rai ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tusianzie Mwanza Mjini, tuanzie Usagara kuelekea Mwanza Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba ushauri huu na rai hii ya Mheshimiwa Silvery Luboja, Mbunge wa Misungwi nimeipokea na nitaifikisha katika jopo la watalaamu, tutaitathmini na kuona kwamba ni namna gani tunaweza kutekeleza *either* kuanzia Usagara kwenda Mwanza Mjini au kuanzia Mwanza Mjini kurudi Usagara, lakini kwa hakika ushauri wake nimeupokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; anasema kwamba kutokana na maendeleo haya mazuri yanayoendelea katika eneo hili yanapelekea umuhimu wa kuifungua Barabara ya kutoka Fulo mpaka Nyambiti mpaka Malya na ni kweli barabara hii ni muhimu ambayo itapeleka muunganiko mpaka Sengerema kwa Mheshimiwa Tabasam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba na yenyewe tunaikamilishia upembuzi yakinifu na mara baada ya kuwa tumekamilisha upembuzi yakinifu wake tutapata gharama halisi na katika lengo lile la kuondosha msongamano katika miji haswa Jiji la Mwanza, barabara hii na yenyewe ni muhimu kwa

hivyo tutaipa umuhimu kwanza tukishapata hizo gharama, tukishajua hizo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaingia katika mkakati wa kutafuta fedha na baadaye kutangazwa zabuni kumpata mkandarasi na hatimaye hatua kwa hatua kuanza kuitekeleza kwa kuijenga. Nikupongeze sana tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Silvery Luboja kwa maswali haya mazuri ya wananchi wa pale Misungwi na Jiji la Mwanza kwa ujumla wake, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kwa kutupatia pesa kwa ajili ya kufanya ukarabati mdogo katika barabara inayotoka Mchinga – Kilolambwani – Mvuleni hadi Kijiweni na kiasi hicho cha pesa walichotupatia ni takribani ya shilingi milioni 100, sasa hizi shilingi milioni 100 haziwezi kutosheleza na tuliomba pesa takribani kama shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuitengeneza hii barabara ambayo ilikuwa imeharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kujua lini Serikali itatupatia hizo pesa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa hiyo barabara ambayo inahusisha kata tatu, ahsante sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimepokea shukrani hizi alizozitoa za wananchi wa Mchinga kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan; na mbili ombi lake la kupata hizi fedha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nilipokee jambo hili na niwahimize watalaam wetu ya kwamba fedha yoyote itakayokuwa imepatikana kuelekea katika Mkoa wa Lindi, tutaipa kipaumbele barabara hii kwa maana kwamba kwenda kutimiza ombi hili la wananchi wa Mchinga. Nisisitize na huu ndiyo msimamo wetu kwamba fedha ndogo tunayoipata ama fedha kidogo tunayoipata watalaam wote wa barabara ikiwa ni pamoja na *TANROADS* na hata wale wa *TARURA* ni muhimu sana kuhakikisha kwamba fedha hiyo kidogo itumike kikamilifu katika maeneo yale korofi yanayoweza kuwa ni chanzo kikubwa cha wananchi kutoweza kupata *access* ya kwenda sokoni, hospitali na katika huduma zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fedha ile kidogo inayopatikana itumike vizuri kuondoa vikwazo kwa maana *bottleneck* ili wananchi/wakulima wa ufuta, wakulima wa korosho na mbaazi na mazao mengine wakiwa ni pamoja na wananchi wa pale Mchinga wawe na uwezo wa kutumia barabara wakati wowote bila ya kusahau kuzingatia viwango vya ubora vya ujenzi wa barabara zetu kwa kuwa zinajengwa kwa fedha za walipa kodi wa Taifa hili, mnatakiwa kuhakikisha kwamba ni lazima ziwe ni barabara zenye viwango vya ubora, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, sisi tuna barabara inayoanzia Igawa mpaka Tunduma. Barabara hii ni barabara inayoenda kutuunganisha nchi ya Zambia, magari yana…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila tafadhali ongeza sauti na ikaribie *microphone* ili tuweze kukusikia.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahaa, *okay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii magari ni mengi kiasi kwamba yanatuelemea na haina barabara ya mchepuko…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa barabara ipi? Anza swali lako.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara inaitwa Igawa – Tunduma; barabara hii ni barabara ya msingi ambayo inaenda kuunganisha na Zambia. Barabara hii haina barabara ya mchepuko njiani, magari ni mengi, ajali ni nyingi na changamoto ni nyingi. Serikali kweli imeweka dhamira ya kujenga barabara nne, lakini hatuoni ule u-*serious* wa Serikali kuanza ujenzi wa barabara hiyo hususan kutoka Mloo kuelekea Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni upi mkakati wa Serikali kuanza ujenzi haraka katika Mji wa Tunduma ili kutunusuru na ile foleni? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Mwandabila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwondoe hofu najua hii ni barabara ya kiuchumi ni barabara kuu inabeba uchumi wetu. Mafanikio ya Bandari ya Dar es Salaam huwezi kuyataja bila ya kuitaja Barabara ya Igawa – Tunduma kwa sababu zaidi ya nusu ya mzigo unaotoka Bandari ya Dar es Salaam unapita barabara hii kwa lengo la kupeleka mizigo upande wa Zambia na upande wa Kongo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iko *very serious,* naomba nimhakikishie Mbunge na Wabunge wote iko *very seriously* na ushahidi wa *seriousness* hiyo pale ambapo yeye atakuwa shahidi na Wabunge wa Mkoa wa Songwe watakuwa mashahidi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba alifanya ziara na alitoa maagizo ya kuhakikisha ya kwamba tunatanua barabara eneo lile la

Tunduma kwa sababu ni eneo ambalo limekuwa likikabiliwa na msongamano mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa ya kwamba moja; Wizara ya Ujenzi tulipokea maelekezo yale ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; mbili, tuliweka mkandarasi pale, mkandarasi wa hapa nyumbani Kampuni ya Narumo iko pale; tatu, mkandarasi alikwishakuanza kufanya kazi ya upanuzi wa barabara ile mwanzo ilikuwa ni meta 700 lakini mara baada ya kufanya usanifu tumefanya zaidi ya meta 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ni zaidi ya kilometa moja ni barabara nne, mbili zinaingia na mbili zinatoka na hivi sasa katika lile eneo utaona kuwa kuna pametanuka sana; na nne, katika jambo hilo ni kwamba mradi umeishafika zaidi ya 40% mara baada ya kupata fedha taslimu za mradi ule zote shilingi bilioni sita na milioni mia nne zimepelekwa pale Tanduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwalike Mheshimiwa Neema Mwandabila na Wabunge wa Mkoa wa Songwe wafanye ziara ya kwenda kukagua waone kazi kubwa na nzuri ambayo inafanywa pale Tunduma itakayoondoa ule msongamano uliokuwa siyo wa lazima katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango mkubwa tayari *feasibility study* ya mwanzo imeshawasilishwa na hivi sasa tumepokea *feasibility study* ya pili ya Kampuni ambayo tunakwenda kufanyanalo *PPP,* Kampuni la *CCECC* ambalo imeonesha *interests* ya kuijenga barabara ile katika mfumo wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo sasa mara baada ya kukamilisha kazi hiyo ya hatua hizi mbili za *feasibility study* (upembuzi yakinifu) tutakuwa tunatarajia kwenda katika hatua inayofuata ili kusudi tuweze kufanya mradi ule wa kielelezo wa uchumi wa Taifa letu katika Mfumo wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mwandabila na Wabunge wote na niendelee kumkaribisha

kwenda kuona kazi kubwa na nzuri inayofanywa pale Tunduma ya marekebisho ya lile eneo na kwa hiyo, malori yaliyokuwa yaki-*park* njiani kwa sababu ya foleni, sasa yatapata unafuu mkubwa sana wa kuweza kupita katika eneo lile, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini ujenzi wa barabara ya mzunguko *(ring road)* katika Jimbo la Tabora Mjini utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya mzunguko ya Tabora *(Tabora Bypass)* imetamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Nimpongeze Mheshimiwa Hawa Mwandabila kwa ufuatiliaji wake na tayari...

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani ni Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora kwa ufuatiliaji wake wa karibu sana wa *Bypass* hii ya Tabora na siyo *bypass* ya Tabora peke yake. Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Ilani ya Uchaguzi imezingatia Miji yetu yote ukienda Babati utakuta kwamba barabara kuu inapita katikati ya mji, ukienda Morogoro pamoja na kwamba ile ilikuwa ni *bypass* lakini sasa inaonekana kuwa inapita katikati ya mji na miji mingine ikiwa ni Singida na kadhalika, yote malori yanakatisha katikati ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi kufuatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi tumelizingatia jambo hili kwamba ni lazima tuondoshe misongamano katikati ya mji kwa kutengeneza *bypass.* Hivyo hii ni moja ya kazi tutakayoifanya kwa kufanya upembuzi yakinifu na wa kina tupate gharama za kufanya hivyo pale Tabora Manispaa na baadaye kutafuta fedha na hatimaye kuitengeneza ile *bypass*

ya Tabora ili kusudi tuuache mji uwe ni mji wa kibiashara na huduma na malori yaweze kupita pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Tabora kwamba jambo hili tumelipokea, tunalifanyia kazi na tumpongeze sana kwa ufuatiliaji wake kwa maslahi mapana ya wananchi wa Tabora na nchi yetu kwa ujumla wake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Ujenzi tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Naomba niwatambulishe kwenu wageni walioko Bungeni asubuhi ya leo na tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wapo wageni 21 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum ambao ni Kamati ya Maendeleo ya Kata ya *Mbalizi Road,* Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 14 wa Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ambao ni viongozi wa Shule ya Msingi Nyabusalu ambayo imeongoza kitaifa mtihani wa darasa la nne mwaka 2025 kutoka Kahama, Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 61 wa Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele ambao ni Kamati ya Ujenzi ya Basilika ya Kanisa Katoliki Kizota, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 47 wa Mheshimiwa Mhandisi Kija Limbu Ntemi ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Biashara *(CBE),* Kampasi ya Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 66 na walimu 11 kutoka Shule ya Sekondari Mwanzi, Manyoni, Mkoani Singida. *(Makofi)*

Pia, wapo wanafunzi 160 na walimu 10 wa Shule ya Msingi *St. Theresa* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wetu wote karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nilete tangazo kwenu limetolewa na Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Konga ya WAVYUU kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilala wapo katika viwanja vya Bunge kwa ajili ya kuonesha shughuli mbalimbali wanazozifanya. Hivyo basi, Wabunge wote mnakaribishwa kufika katika eneo hilo na kupata maelezo zaidi kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Konga hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naomba kuahirisha Shughuli za Bunge…

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Hadi kesho saa tatu asubuhi.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, …

*(Saa 5.20 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 04 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*